# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**

**S. L.P. 38**
**GEITA**
**Simu: 028-2520004**
**Nukushi: (028) 2520040**
**Baruapepe:** rbcgeita@pccb.go.tz
**Website**: www.pccb.go.tz


**GEITA – APRILI, 2022.**

## TAKUKURU GEITA YAFUATILIA UTEKELEZAJI WA MIRADI YENYE THAMANI YA ZAIDI YA SHILINGI BILIONI 18

**Ndugu Wanahabari,**
Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutukutanisha leo hii kwa ajili ya kuwapeni taarifa ya kazi zilizotekelezwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Geita, katika kipindi cha miezi mitatu kuanzia Januari hadi Machi, 2022. Taarifa hii inatokana na ofisi ya Mkoa na wilaya zake ambazo ni Chato, Bukombe, Mbogwe na Nyang'hwale, ambapo kazi mbalimbali zimetekelezwa kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329 Marejeo ya Mwaka 2019, kwa lengo la kukuza utawala bora na kuondoa rushwa.

Kazi hizi zimetekelezwa kupitia njia ya Uzuiaji wa vitendo vya rushwa kwa kuziba mianya inayochangia uwepo wake; Uelimishaji umma ili kuchagiza ushiriki wa wadau mbalimbali katika vita dhidi ya rushwa; Pamoja na kuchukua hatua dhidi ya wahalifu wanaojihusisha na vitendo vya rushwa na makosa yahusianayo kwa kufanya chunguzi zinazopelekea kufungua mashtaka Mahakamani kwa kibali cha Mkurugenzi wa Mashtaka nchini.

### UZUIAJI RUSHWA
**Ndugu Wanahabari,**
Katika kipindi cha Januari hadi Machi, 2022, TAKUKURU Mkoa wa Geita imefanya kazi ya Uzuiaji wa vitendo vya Rushwa kwa kuziba mianya inayochangia uwepo wake kwa kuendelea na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa lengo la kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za umma.

Jumla ya Miradi ya Maendeleo **19** (Katika sekta za Afya, Elimu, Ujenzi, Maji na Kilimo) yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 18.67** ilifuatiliwa. Thamani hii ni kwa mujibu wa mikataba ya miradi husika.

Miradi **15 yenye thamani ya shilingi Bilioni 18.3** ilibainika kuwa na mapungufu ya kutozingatiwa kwa vigezo na masharti yaliyoainishwa kwenye michoro na BOQ; Kukosekana kwa usimamizi thabiti kutoka kwa wataalamu wa Halmashauri; pamoja na baadhi ya mafundi walioshinda zabuni za ujenzi kutokuonekana katika eneo la mradi na kuwaacha mafundi wasaidizi pasipo usimamizi wala maelekezo eneo la ujenzi. Baada ya ufuatiliaji huu, wahusika walishauriwa namna bora ya kuboresha utekelezaji wa miradi hiyo kupitia vikao kazi.

Miradi **4** katika Sekta ya Elimu **yenye thamani ya sh. Milioni 340** ilionekana kuwa na viashiria vya ufujaji na ubadhirifu wa fedha, hiivyo uchunguzi umeanzishwa na unaendelea.

Katika **udhibiti** tumefanya **chambuzi 5** za mifumo ya viashiria vya rushwa ya ngono katika Sekta za Afya, Elimu na Madini, ambapo mianya ya rushwa ilibainishwa na kwa kupitia warsha na vikao vya wadau 4 tulikaa na kujadili matokeo ya chambuzi zetu na kuwekeana maazimio ya namna bora ya kuondokana na mianya hiyo ya rushwa.

**UELIMISHAJI UMMA**

**Ndugu Wanahabari,**

Katika kipindi cha Januari hadi Machi, 2022, Elimu ya mapambano dhidi ya rushwa imetolewa katika makundi mbalimbali ili ***kuhamasisha umma kushiriki mapambano dhidi ya Rushwa***. Mbinu mbalimbali za kuelimisha zimetumika ambapo jumla ya kazi **180** zimefanyika (zikiwemo Semina 54, Mikutano ya hadhara 46, uimarishaji wa klabu za wapinga Rushwa 62 katika Shule za Msingi na Sekondari, Utoaji wa taarifa kwa vyombo vya habari 11 Maonesho 3, vipindi vya redio 2, Mkutano na waandishi wa habari 1 pamoja na kugawa machapisho mbalimbali kwa wananchi yenye ujumbe wa kukemea vitendo vya rushwa).

**Vilevile, Wadau wameendelea kushirikishwa** katika kuzuia na kupambana na rushwa kwa kufanya yafuatayo;
**Kwanza**, tumeshirikiana na Mahakama katika kuadhimisha Wiki ya Sheria nchini ambapo elimu ya mapambano dhidi ya rushwa hasa katika huduma ya utoaji haki kupitia banda letu la maonesho ilitolewa kwa wananchi wote waliotembelea banda na kuweza kutatuliwa kero zao.

**Pili**, tumeshiriki maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani mkoani Geita katika viwanja vya CCM Kalangalala ambapo kupitia banda letu, elimu ya mapambano dhidi ya rushwa, hususani rushwa ya ngono inayowaathiri zaidi wakina mama ilitolea kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mji Geita.

**Tatu,** tumeendelea na mpango wa kuwashirikisha vijana wa Skauti Tanzania katika mapambano dhidi ya rushwa kwa kuwaelimisha katika misingi ya Uadilifu, Uwajibikaji na Uzalendo kupitia mkakati wa pamoja wa TAKUKURU NA SKAUTI (TAKUSKA) kupitia mwongozo wa ushirikiano huo.

**Nne**, tumetoa elimu ya Rushwa na Maadili kwa watumishi wa Sekta za Umma na Binafsi kwa kuwahimiza kuwa waadilifu katika utekelezaji wa majukumu yao kwa kujiepusha na ubadhirifu, wizi pamoja na matumizi mabaya ya ofisi za umma.

## UCHUNGUZI NA HUDUMA ZA SHERIA

**Ndugu Wanahabari,**

Katika kipindi cha Januari hadi Machi, 2022 tumeendelea kupokea malalamiko na kisha ***kufanya Uchunguzi na kupelekea kufungua mashtaka ya tuhuma za Rushwa Mahakamani kwa kibali cha Mkurugenzi wa Mashtaka nchini.***

- Tumepokea taarifa na malalamiko **75** ambapo taarifa zilizohusu rushwa ni **40** na **35** hazihusiani na rushwa hivyo zimetolewa ushauri na kuelekeza walalamikaji mahali sahihi pa kupeleka malalamiko yao.
- Sekta iliyoongoza kwa kulalamikiwa ni Serikali za Mitaa (32), Binafsi (10), Fedha (7), Elimu (8), Misitu (3), Sekta ya Madini (3), Afya (3), Ardhi (3), Polisi (2), Mahakama (1), Ujenzi (1) na zilizohusu Siasa taarifa 2.
- **Taarifa 40** zilizohusu rushwa zimefunguliwa majalada ya uchunguzi ambapo majalada ya uchunguzi **29** yanaendelea kufanyiwa kazi**,** majalada **6** yametolewa ushauri na majalada **5** uchunguzi wake umekamilika.
- Kesi zilizofunguliwa mahakamani ni **2** na kufanya jumla ya kesi zilizoendeshwa mahakamani kufikia **26**
- **Kesi 4** zilitolewa maamuzi na Jamhuri ilishinda katika kesi zote.

**Ndugu Wanahabari,**

Kazi zote hizi zimeweza kutekelezwa ikiwa ni mafanikio ya ushirikiano tunaoupata kutoka kwa wadau mbalimbali katika mapambano dhidi ya rushwa, mkiwemo ninyi waandishi wa habari. Aidha wanachi wamekuwa na mwitikio chanya kupitia elimu wanayopewa kwa kuwafichua wanaojihusisha na vitendo vya rushwa,

kutoa ushahidi mahakamani na kutambua wajibu wao wa kusimamia miradi ya maendeleo kwa kushirikiana na Serikali.

**Ndugu Wanahabari,**
Katika kipindi cha Januari hadi Machi, 2022 ofisi iliendelea na utaratibu wa kusikiliza kero za wananchi kwa utaratibu wa TAKUKURU INAYOTEMBEA ambapo **mikutano 06** ilifanyika katika maeneo mbalimbali.

Kupitia mikutano hiyo wananchi walielimishwa kuhusu athari za rushwa na pia waliuliza maswali na kupewa ufafanuzi kwa lengo la kutatua kero walizokuwa nazo.

**Ndugu Wanahabari,**

**MKAKATI WA APRILI HADI JUNI, 2022**

- Tutaendelea KUZUIA VITENDO VYA RUSHWA kwa kutatua kero za wananchi, kutoa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa pamoja na kuendelea kuwashirikisha vijana wa Skauti katika mapambano dhidi ya rushwa kupitia ushirikiano wa TAKUKURU NA SKAUTI (TAKUSKA).
- Tutaendelea kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo
- Tutaendelea kuhimiza watumishi wa Sekta za Umma na Binafsi kuwa waadilifu katika utekelezaji wa majukumu yao.
- Tumetenga siku moja kila mwezi ambayo tutakuwa tunawafuata wananchi walipo kupitia utaratibu wa TAKUKURU INAYOTEMBEA, ili kusikiliza na kutatua kero zao dhidi ya rushwa.
- Tutaendelea kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo hasa ile ya kimkakati pamoja na ya Sekta za Afya na Elimu.
- Tutafuatilia utekelezaji wa maazimio tuliyokubaliana na wadau katika warsha za kujadili mianya ya rushwa iliyobainishwa katika chambuzi tulizokwisha zifanya ikiwa ni pamoja na kuendelea kusimamia utatuzi wa kero zilizoibuliwa kupitia majaribio ya mpango wa TAKUKURU - RAFIKI.

Wito wetu kwa wananchi wa mkoa wa Geita, ni kwamba waendelee kushirikiana na TAKUKURU katika kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika maeneo yao na pia kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa kwa vitendo. Wajihadhari na watu wanaojifanya Maafisa wa TAKUKURU na wasisite kutoa taarifa za vitendo vya rushwa katika ofisi za TAKUKURU kwa kupiga simu bure nambari 113, *113# au kutuma ujumbe mfupi wa maneno kwenda namba 113.

Vile vile, tunawaasa watumishi wa Sekta za Umma na Binafsi mkoani Geita, wawe waadilifu katika utekelezaji wa majukumu yao kwa kujiepusha na ubadhirifu, wizi pamoja na matumizi mabaya ya ofisi za umma ili kuwaondolea kero ya rushwa wananchi wetu pindi wanapohitaji huduma kutoka kwao.

Ahsanteni kwa kunisikiliza. Sote tuseme ***"KUPAMBANA NA RUSHWA NI JUKUMU LANGU"***

IMETOLEWA NA:
Leonidas R. Felix,
**Mkuu wa TAKUKURU (M) Geita**,
Simu: 0738 150078